



Maswali

1. Mbona Mungu alimjaribu Ibrahimu?
2. Mungu aliambia Ibrahimu afanye nini?
3. Ibrahimu alifanya nini?
4. Walisafiri kwa muda gani?
5. Walienda wapi?
6. Isaka na Ibrahimu walibeba nini wakienda mlimani?
7. Isaka aliuliza Ibrahimu eti nini? Ibrahimu alijibu nini?
8. Nini ilifanyika wakati Ibrahimu alitaka kuua Isaka?
9. Ibrahimu alitoa sadaka gani badala ya Isaka?
10. Yesu anatimiza ahadi iliyoahidiwa na Mungu kwa Ibrahimu

Majibu

1. Mungu alitaka kujua kama Ibrahimu anampenda zaidi ya kila kitu.
2. Mungu aliambia Ibrahimu amtolea mwanawe wa pekee Isaka kama sadaka ya kuteketeza.
3. Ibrahimu alienda kumtoa Isaka kama sadaka siku iliyofwata.
4. Walisafiri kwa siku tatu.
5. Walienda mlimani kwa nchi ya Moria.
6. Isaka alibeba kuni. Ibrahimu alibeba kisu na mwenge wa moto.
7. “Wapi kondoo wa kuteketezwa kama sadaka? Mungu atapeana huyo kondoo.?”
8. Malaika alimwambia asimuumize Isaka kwa sababu Mungu sasa amejua kwamba anampenda kuliko kila kitu.
9. Ibrahimu aliona kondoo mume ameshikwa kwa kichaka na akamtolea Mungu sadaka.
10. Yesu alitoa uhai wake ili dhambi zetu zisamehewe. Kila mtu atafurahi kwa Ufalme wa Mungu Yesu akirudi.

6 Mungu anamjaribu Ibrahimu

Marejeo

Mwanzo 22 : 1 – 19

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Ibrahimu alipenda na kumtii Mungu hata kuku-bali kumtolea mwanawe wa pekee. Alikuwa na imani kubwa kwa Mungu.

Maneno maalum

- 6.1 Isaka + Mungu anajaribu + Ibrahimu + chukuwa mwana wa pekee + Moria + ua + Ibrahimu anakadhabika
- 6.2 Ibrahimu + anapenda Mungu + anatii + anasafiri + Moria
- 6.3 Ibrahimu + Isaka + panda + kuni + kisu + moto + wapi mwana kondoo + Mungu atapeana
- 6.4 Madhabahu + Isaka alifungwa + kisu cha kuua + malaika + usimuumize + kondoo mume kwa kichaka + badala ya sadaka ya kuteketezwa.
- 6.5 Mungu akafurahi + ahadi + Yesu mwana wa Mungu + kufa kwa ajili ya dhambi zetu + Ufalme wa Mungu duniani.

6.1 Ibrahimu na Sara walifurahi sana mwanao Isaka alipozaliwa. Isaka alikua akawa kijana wa nguvu na kuwa wa furaha kubwa kwao.

Siku moja Mungu alimjaribu Ibrahimu ili ajue kama anampenda kuliko kitu kingine chochote. Mungu alitaka kuona kama anamwamini kwamba atatimiza ahadi zake.

Mungu alimwambia, “Chukua mwanao, mwanao wa pekee, Isaka, unayempenda. Enda kwa nchi ya Moria, kwa mlima mmoja nitakao kuonyesha. Ua Isaka ili unitolee kama sadaka ya kuteketeza.”

Ibrahimu anakadhabika sana. Anaweza kuaje mwanawe wa pekee? Isaka alikuwa amemletea furaha kubwa. Alikuwa ameongoja Isaka azaliwe kwa muda. Ahadi za Mungu zingetimizwa namna gani ikiwa Isaka atakufa?

6.2 Lakini Ibrahimu alipenda Mungu sana. Alipenda Mungu zaidi ya kila kitu. Ibrahimu aliamini kwamba Mungu anajua yote. Alitii Mungu. Ibrahimu aliamka asubuhi mapema sana. Alitandika punda. Alichukua watumishi wake wawili, kuni, moto na kisu. Akaondoka pamoja na Isaka.

Baada ya kusafiri kwa siku tatu, Ibrahimu aliona kwa umbali mlima uliokuwa kwa nchi ya Moria. Hapo ndipo Mungu alimwambia aende. Kwa hivyo Ibrahimu na Isaka waliaacha watumishi na punda. Waliwaambia kwamba walikuwa wanaenda mlimani kuabudu Mungu halafu watarudi.



6.3 Ibrahimu na Isaka walianza kupanda mlima. Isaka alibeba kuni ya kuchomea. Ibrahimu alibeba kisu na mwenge wa kuwasha.

Walipokuwa wakipanda mlima Isaka aliuliza, “Baba, tuna kuni ya kuwasha, lakini wapi mwana kondoo wa sadaka?” Ibrahimu alikuwa na huzuni sana. Alijibu Isaka, “Mwanangu, Mungu ataleta mwana kondoo wa sadaka.” Waliendelea na safari.

6.4 Mwishowe walifika mahali penye Mungu alikuwa ameambia Ibrahimu. Ibrahimu alianza kujenga madhabahu ya kumtolea Mungu mwanawe Isaka. Alipanga kuni kwa taratibu. Na huzuni mwingi aligeuka akafunga Isaka na kumweka kwa madhabahu.

Alipoinua mkono wake ili amue Isaka kwa kisu, malaika kutoka mbinguni alimwita. Malaika alisema, “Ibrahimu, Ibrahimu, usimumize kijana. Sasa najua kwamba unampenda Mungu.”

Ibrahimu alifurahi sana alipofungua Isaka na kumteremsha kutoka kwa madhabahu. Ibrahimu aliona kondoo mume aliyekuwa amenaswa kwa kichaka. Ibrahimu akamtoa kondoo awe sadaka wa kuteketezwa badala ya Isaka.



6.5 Mungu alimwambia Ibrahimu kwamba alimfuhia kwa sababu alimtii. Mungu alijua kwamba Ibrahimu alipenda sana na alimwaamini. Tena Mungu akamwaahidi kwamba atakuwa taifa kubwa na mmoja wa uzao wake atawafurahisha watu wote ulimwenguni.

Yesu ndiye huyu mzao wa kipekee. Yesu alikuwa mwana mpendwa wa Mungu. Yesu alitoa uhai wake ili tusamehewe dhambi zetu na tuwe na tumaini la kuishi milele katika Ufalme wa Mungu hapa duniani.